

(NBAA)
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU
TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

MATOKEO YA MITIHANI YA UHASIBU ILIYOFANYIKA NOVEMBA 2017
NA TARATIBU ZA MITIHANI YA FEBRUARI 2018 NA MEI 2018

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania inataarifu umma ya kwamba matokeo ya mitihani mbalimbali ya uhasibu iliyofanyika mwezi wa Novemba 2017 kwa ngazi za cheti cha Utunzaji Hesabu (Accounting Technician) na Taaluma ya Uhasibu (CPA), yapo kwenye maandalizi na pindi yatakapokuwa tayari muda wowote kuanzia sasa yatatangazwa. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo Ndogo za Usimamizi wa Mitihani na Mafunzo za mwaka 2014 kifungu cha 21 kinaeleza ya kwamba matokeo hutangazwa punde yatakapokuwa tayari na kuthibitishwa.

Kwa tangazo hili tunaomba kuufahamisha umma kwamba;

- (1) Watahiniwa wote waliofanya mitihani katika ngazi mbalimbali kuwa na subira katika kipindi hiki ambapo matokeo hayo yapo kwenye maandalizi kwa mujibu wa Sheria hizo.
- (2) Kwa wale Watahiniwa wanaoanza (wapya) mwisho wa kujiandikisha kwa ajili ya mitihani ya Mei 2018 ni tarehe **15 Februari 2018**.
- (3) Kwa Watahiniwa wanaoendelea ambao hawakufanya mitihani ya mwezi Novemba 2017 wao pia taratibu za usajili kwa ajili ya mitihani ya mwezi Mei 2018 zinaendelea kama kawaida na mwisho wa usajili ni tarehe **15 Februari 2018**.
- (4) Kwa wale watahiniwa waliofanya mitihani mwezi Novemba 2017 wanaruhusiwa kujisajili kwa ajili ya mitihani kwa **somo/masomo ambayo hawakuyafanya katika mitihani ya mwezi Novemba 2017** na mwisho wa usajili ni tarehe 15 Februari 2018.
- (5) Kwa Watahiniwa ambao walikuwa wamebakiza masomo machache ili kuingia ngazi (level) inayofuata **wanaruhusiwa** kujisajili kwa ajili ya masomo ya ngazi inayofuata (ATEC I kwenda ATEC II, Foundation kwenda Intermediate au Intermediate kwenda Final) na mwisho wa usajili ni **tarehe 15 Februari 2018**.
- (6) Kwa Watahiniwa waliyofanya mitihani ya mwezi Novemba 2017 ambao masomo waliyofanya yalikuwa ya mwisho ili kutunukiwa Cheti cha ATEC II au CPA (T), tarehe ya mwisho ya kujisajili kwa ajili ya mitihani ya mwezi Mei 2018 itatangazwa mara baada ya matokeo.
- (7) Usajili kwa ajili ya mitihani ya Mid-session Februari 2018 kwa ajili ya masomo ya A5, B4 na C4 unaendelea hadi tarehe **23 Februari 2018**.

Umma unaombwa kuzingatia tangazo hili. Endapo mtu yeyote atakuwa na jambo linalohitaji ufafanuzi zaidi asisite kuwasiliana na Bodi kwa anwani iliyotajwa hapa chini.

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza na tunawatakia maandalizi mema ya mitihani ya mwezi Februari na Mei 2018.

MKURUGENZI MTENDAJI
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU (NBAA)
MHASIBU HOUSE
MTAA WA BIBI TITI MOHAMED
S.L.P 5128
DAR ES SALAAM
SIMU: +255 22 2211890-9
Nakushi: +255 (22) 2151746, Barua pepe: info@nbaa.go.tz
Tovuti: www.nbaa.go.tz